.

# OFISI YA RAIS

## SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

***27 Mei, 2025***

### MABADILIKO YA TAREHE NA MAHALI PA USAILI WA MAHOJIANO

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anawajulisha waombaji kazi wote waliopangiwa kufanya usaili wa mahojiano TABORA, kituo cha usaili kitakuwa **SHULE YA SEKONDARI MIRAMBO** badala ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora kama ilivyooneshwa kwenye tangazo la awali.

Kwa wasailiwa wote wa kada za Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) mnajulishwa kuwa kituo cha usaili wa mahojiano kitakuwa ni **Ofisi za Sekretarieti ya Ajira Makao Makuu (Dodoma**).

Aidha, kwa wasailiwa wa kada za Mkufunzi Msaidizi wa Ardhi (Land Management ,Evaluation and Registration), Mkufunzi Msaidizi wa Ardhi (Graphics Arts and Printing) , Mkufunzi II (Environmental Management), Mkufunzi Msaidizi wa Ardhi (Cartographer), Mkufunzi Msaidizi wa Ardhi -Geographical Information System (GIS), Mkufunzi Msaidizi wa Ardhi(Land Surveyor), Mkufunzi II (Architect) na Fundi Sanifu II-Upimaji Ardhi (Land Technician Survey II) mnajulishwa kuwa usaili wa mahojiano utafanyika tarehe **05 Juni,2025**.

Aidha,maelekezo mengine yatabaki kama yalivyo kwenye tangazo la awali la kuitwa kwenye usaili.

**Imetolewa na :**
**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**